It is known that the big rainforest in West Africa was widespread throughout the whole of Africa. Because of differences in climatic conditions about 10 million years ago, the East African forest was separated from West African forest. As a result of drought and the development activities of people, these forests have been separating and becoming isolated, surrounded by dry scrub/woodland areas, estates and residential areas. These mountains have also been called the 'Galapagos Islands' of Africa due to their isolation and the presence of different living organisms that are only found here and nowhere else in the world, e.g. there are 16 genera of plants and 20 of 21 species of house flowers (African violets) that are found only in the Eastern Arc mountains.

### **4. *What are the importance of Eastern Arc mountain forests?***

Geographically these mountains have forests which are very important in Tanzania for conserving water sources (rivers), for providing a resource to people living in big cities such as DSM, Tanga, Morogoro etc. and for hydroelectric power for generating electricity e.g. Pangani, Kihansi. There are big dams (Mtera, Mindu) important for fishing, irrigation and home uses. People living in these areas have daily needs from these forests – water, charcoal, firewood, drugs, poles and timber. Also these forests have been important for the conservation of the environment and regulation of air, contributing a lot to rainfall. So these forests are the spinal chord of the country and heritage of future generations. In the world they are the 24<sup>th</sup> biodiversity hotspot.

### **5. *Do you know that these forests are in danger of disappearing?***

The sad/worrying thing about these mountains' forests are that they have been intensively cut for timber and other uses together with bushfires. Although there is protection, illegal harvesting of timber is a big problem. Also, many areas have been cleared for cash crops or cultivation such as tea or coffee. These areas have fertile soil. Other development activities affecting these forests include overgrazing, mining, road constructions, railways, illegal hunting etc. Population increase is growing simultaneously with the demand for forest products and resources and endangering the sustainability of forests.

### **6. *What are the factors affecting the forests?***

Among the forms of forest destruction (some happening for short and some for long periods of time) are the following:

- i. soil and land degradation
- ii. drought
- iii. floods
- iv. destruction of water sources (drying out)
- v. invasion of foreign/invasive species
- vi. invasion of other living organisms e.g. animals, insects, birds, plants etc.
- vii. Climate change e.g. temperature increases, ozone gases

***7. Are there any conservation measures being practised in the Eastern Arc mountains?***

At present the Eastern Arc mountains are known clearly by biologists and researchers, but we have seen there is a big need to educate Tanzanian people to know what is going on concerning their own biodiversity. Environmental education has been given to people near to these mountains aiming to improve environmental degradation. The government and NGOs have started conservation efforts by collaboration with local people living adjacent to forest areas. These efforts will increase awareness to plant trees in their shambas for the purpose of their daily needs. Also these efforts have started to educate peasants about farm forestry and agroforestry.

---

## 7.2: Minutes of Mlinga Environmental Committees Meeting (Kiswahili)

*Katibu wa kikao - Frank S. Mahenge*

### MAFUNZO YA ELIMU YA MAZINGIRA 9/11/2001

Wajumbe waliohudhulia

No.	JINA	CHEO	ATOKAKO
1	Mr. Thabiano	M/kiti	Magula
2	Alphonse Msenga	Mjumbe	Misozwe
3	Albert Ntemi	B/miti (EUCAMP)	Maramba
4	Ernest Michael	Mjumbe	Kanyalika
5	Dismas Mhando	Mjumbe	Misozwe
6	William J. Kumwaga	Mjumbe	Misozwe
7	Peter Semgodo	Mjumbe	Magula
8	James Mlima	Mjumbe	Misozwe
9	Jullius Usingu	Mjumbe	Mwembeni
10	Sylvester Mukanda	M/kiti	Magula
11	Sturt Bakari	Mjumbe	Mwembeni
12	Sylvester Juma	Mjumbe	Mwembeni
13	Andrew D. Kalage	M/Mazingira	Mwembeni
14	Matoe Charles Hiza	Katibu/mz.	Mwembeni
15	Luka H. Y. Kingazi	Katibu/Mz	Magula
16	Edmund Challenge	Mjumbe	Misozwe
17	Rashid M. Mtulu	Mjumbe	Mwembeni
18	Francis M. Mdachi	Katibu/Mz	Misozwe
19	Joyce Tupa	Mjumbe	Misozwe
20	Beatrice Mlenga	Mjumbe	Misozwe
21	Jestina Ernest	Mjumbe	Magula
22	Grace Raphael	Mjumbe	Magula
23	A. B. Mbio	M/Kiti	Misozwe
24	Matiko Wambura	APM-eucamp	Tanga
25	Selemani Hamadi	B/Miti-eucamp	Misozwe
26	Francis Kiondo	Frontier-Tz	Tanga
27	Frank S. Mahenge	Frontier-Tz	Amani
28	Adam Murphy	Frontier-Tz	Uingereza
29	Susannah Hall	Frontier-Tz	Uingereza

### MPANGO WA ELIMU KWA KAMATI ZA MAZINGIRA NOVEMBA 9, 2001

#### Utafiti wa viumbe adimu katika msitu wa Hifadhi Mlinga (East Usambara Biodiversity Surveys).

Mkutano wa mafunzo uliojumuishia kamati za mazingira za vijiji vitatu Misozwe, Magula na Magoroto-Mwambene ulioandaliwa na watafiti ulifunguliwa mnamo saa 3:30 na Bwanamiti wa eneo hilo. Lengo kuu la mkutano ilikuwa ni kutoa matokeo ya utafiti kwa jamii inayozunguka hifadhi hii kwa kutumia njia ya elimu ya mazingira. Mkutano ulifanyika kwenye kambi ya utafiti eneo la Mpakani, Misozwe.

*Agenda za mkutano zilikuwa kama ifuatavyo:*

1. Historia ya kazi za utafiti
2. Mgawanyiko wa safu ya milima ya ukanda wa Mashariki.

3. Hifadhi ya misitu ya Usambara Mashariki
4. Umuhimu wa utafiti katika misitu ya Usambara Mashariki
5. Vitu vinavyofanyiwa utafiti ndani ya misitu ya hifadhi.
6. Matatizo yaliyoonekana katika misitu wa Mlinga na jinsi ya kuyaepuka na kuyatatua.
7. Maswali ya kujiuliza ili kuuokoa misitu Mlinga (Kama tathmini ya ulewaji wa wajumbe).

Mada ya kwanza ilitolewa na Susannah Hall, ambaye ni kiongozi wa utafiti Frontier-Tanzania. Mtoa mada alianza kwa kuwakaribisha wageni, pamoja na kujitambulisha yeye mwenyewe na shughuli anazosimamia, pamoja na taasisi anazoshirikiana nazo katika kazi ya utafiti wa bioanuai (mfano: TAFORI, Chuo Kikuu Dar es Salaam, EUCAMP).

Pia alieleza sehemu ambazo kazi hii ya utafiti imekwishafanyika kuwa ni Misitu ya Kambai, Longuza, Kwamarimba, Bamba, Manga Segoma, Semdoe, Kwamgumi, Mlungui, Mtai, Amani, Nilo na sasa wapo hapa Mlinga.

Mwisho alieleza lengo la utafiti wa viumbe adimu katika milima ya Usambara Mashariki kwamba ni kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu thamani ya viumbe adimu ndani ya misitu, kutoa mafunzo ya utafitikwa wafanyakazi wa hifadhi na kutoa matokeo ya utafiti kwa jamii kwa kutumia njia ya elimu ya mazingira.

Baada ya mada kutolewa wajumbe walieleza jinsi walivyovutiwa na kazi hizo za utafiti na jinsi walivyokumbukwa kwamba wao pia ni wshika dau. Aidha walishukuru kwa kukutanishwa kwa kamati za mazingira katika vijiji vitatu, kwani walikiri hawajawahi kukutana wala kutambulishana, ukizingatia kwamba hifadhi ya mazingira haina mpaka. Hii ilibainika wakati kijiji cha Misozwe kilipowaomba watu wa Magula kuendelea kuhifadhi chanzo cha maji ambacho ni pekee kwa matumizi yao.

Mada ya pili ilitolewa na Ndugu Albert Ntemi, ambaye ndio kiongozi wa kazi ya utafiti kwa upande wa Mradi wa Misitu Usambara Mashariki. Ilihusu maelezo au ufafanuzi wa safu ya milima ya Usambara Mashariki (the Eastern Arc Mountains).

Alianza kwa kuwafahamisha wajumbe mahali ukanda wa milima hii unapopatikana kwa kutumia ramani. Alitaja majina kama ifuatavyo: Taita Hills (Kenya), Pare Kasikazini, na Kusini, Usambara Mashariki na Magharibi, Ngunguru, Ukaguru, Udzungwa, na Mahenge.

Aidha alifafanua kitu kilichosababisha milima hiyo ionekane kama ilivyo sasa-kwamba ni kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, ukame pamoja na shughuli za maendeleo ya binadamu. Zamani miaka milioni kumi iliyopita misitu hii iliunganika na kuwa mikubwa yenye mvua nyingi sana iliyosambaa kutoka Afrika Magharibi na kuenea Afrika nzima (Tropical Forest).

Mtaalamu huyu aliendelea kueleza umuhimu wa misitu iliyopo katika safu ya milima hiyo kwamba ni kuhifadhi vyanzo vya maji, jamii inaypizunguka hupata mahitaji yake ya kila siku kama maji, kuni, mkaa, dawa, nguzo za kujengea na mbao kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Pia kutengeneza mandari asilia ambayo ni kivutio kikubwa kwa watalii na kwamba huhifadhi ardhi na kurekebisha hali ya hewa. Aliongeza kwamba milima hii ni muhimu sana kiulimwengu; ni ya 24 kuwa na bionuwai nyingi (aina mbalimbali za viumbe hai).

Pia alifahamisha wanamazingira hao kuwa milima hii inakabiliwa na hatari ya kutoweka kutokana na shughuli za binadamu kama upasuaji wa mbao, kilimo, kuchoma moto hovyoy, na matumizi mengine ya ardhi; japo kuna udhibiti lakini uvunaji haramu wa mbao bado ni tatizo sugu.

Mtaalamu alifafanua kwamba baadhi ya madhara ya uharibifu wa miti hutokea baada ya muda mfupi na mengine huchukua muda mrefu kujitokeza. Alizitaja athari hizo kuwa ni pamoja na mmomonyoko wa udongo na maporomoko ya ardhi, kutoweka kwa mimea au viumbe fulani fulani, pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa.

Mwisho mtaalamu alifahamisha juhudi zinazofanyika katika kuhifadhi misitu iliyoko kwenye milima ya ukanda wa Mashariki kutokana na umhimu wake kwa watafiti, wanabiolojia na jamii zinazozunguka milima hiyo. Kwamba "...tumeona na kunahaja kubwa ya kuielimisha jamii nzima ya Tanzania ifahamu kinachoendelea kuhusu bionuwai iliyo hadhina kubwa kwetu," na kwamba wameanzisha mpango kamambe wa Elimu ya Mazingira ambayo imeanza kutolewa kwa wananchi wanaoishi katika milima hii, kuhusu madhara ya kuharibu mazingira asilia. Serikali na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali (NGOs) yameanzisha juhudi za kuishirikisha inayoishi au kupakana na maeneo ya misitu katika kuhifadhi misitu. Mfano kuweka mikakati ya pamoja ya kuwahamasisha wananchi kupanda miti katika mashamba yao kwa ajili ya matumizi yao wenyewe.

Mada ya tatu iliyohusu milima ya Usambara Mashariki ilitolewa na ndugu Albert Ntemi (kiongozi wa bioanuwai EUCAMP). Alieleza kuwa misitu hii ni miongoni mwa misitu ya mvua ya ukanda wa Milima ya Mashariki na ina mimea na wanyama ambao baadhi yao hupatikana hapa tu, na kuwa ni mkati ya misitu yenye thamani katika bara la Afrika. Pia misitu hii ni muhimu katika utoaji wa maji kwa wananchi wa Tanga mjini na baadhi ya wilaya za mkoa huu.

Aidha alieleza mafanikio ya mpango wa utunzaji wa misitu ya Usambara Mashariki kuwa umefanikiwa kuanzisha Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Amani, utafiti wa kibiolojia umeongezeka, na kwamba watu wanaendelea kupata kupata mahitaji ya mazao ya misitu ndani ya misitu hiyo.

Mwisho aliwaeleza wanamazingira hao kuwa wajivunie na utajiri walionao wa misitu hii na waitunze kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo kwa kuzingatia matumizi endelevu.

Mada ya nne iliyohusu umhimu wa utafiti katika milima ya Usambara Mashariki ilitolewa na kiongozi wa bioanuwai EUCAMP Ndugu Albert Ntemi.

Alianza kwa kueleza historia fupi ya kazi ya utafiti katika misitu hii kwamba umeanza tangu mwaka 1995 na kuwa umekuwa na matokeo mazuri kwa kufanikiwa kupata mimea na wanyama adimu. Misitu 13 imeshafanyiwa utafiti kama huu katika misitu ya Usambara Mashariki

Madhumuni ya Utafiti yalikuwa kama ifuatavyo:

- Kutafiti mimea na wanyama ndani ya misitu ya hifadhi.

- kusaidia katika mpango wa baadae wa utunzaji wa misitu
- kutoa mafunzo ya utafiti kwa mabwana- na mabibimiti
- kutoa taarifa ya matokeo ya utafiti na mapendekezo kwa ajiri ya matumizi endelevu.
- kuchunguza uharibifu wa misitu na madhara yake.

Mwisho alifafanua mafanikio ya utafiti kwamba ni pamoja na:

- Mimea na wanyama imeweza kujulikana ambayo ilikuwa haijulikani mwanzo.
- umetoa elimu ya utafiti kwa mabwana- na mabibimiti katika mradi wa Hifadhi Misitu Usambara Mashariki.
- watafiti mbalimbali wamevutiwa na kufaidika na utafiti huu.
- kujulikana zaidi ulimwenguni umhimu wa misitu hii ya Usambara Mashariki kupitia utafiti huu.

Mada ya tano ilihusu vitu ambavyo vinafanyiwa utafiti ndani ya misitu ya Hifadhi. Vitu hivyo vimegawanyika katika makundi makuu mawili ya viumbe hai; Mimea na Wanyama. Mada hii ilitolewa na wataalamu wawili ikianza na mambo ya mimea ambayo ilitolewa na Ndugu Francis S. Mahenge (Afisa Misitu ya Hifadhi).

Alianza kwa kueleza hatua ya kwanza ambayo ni kuugawa msitu kwa mstari maalumu (transect line), na baadaye kufuatia mistari ya katikati yenye urefu wa mita 450 ambapo 'plot' za mimea hupimwa. Baada ya hapo kando ya mistari hiitathmini ya uharibifu hufanyika. Pia miti mikubwa zaidi ya sentimita 10 na baadaye viploti vyenye ukubwa wa mita moja ya ukubwa kwenye kona mimea hupimwa na kutambuliwa na mtaalamu wa mimea . Ambayo haijulikani hutumwa katika vyombo vingine vya utafiti wa miti huko Dar es Salaam, Uingereza, Zimbabwe, Marekani na Ujerumani. Katika kuchunguza uharibifu wa misitu na wanyama, watafiti hupita sehemu zote za misitu na kuangalia uharibifu uliofanya na watu. Mfano: ukataji miti, fito na nguzo, uchanaji mbao, uwindaji haramu wa wanyama na nyuki, na uchomaji moto ovyo.

Sehemu ya pili ya mada ya tano upande wa wanyama iliandaliwa na Ndugu Francis Kiondo (Mtafiti Msaidizi). Aliwataja wanyama wanaofanyiwa utafiti kuwa ni Panya, popo, vyura, nyoka, mujusi, ndege, konokono, na wadudu kama vile vipepeo na jongoo.

Alieleza jinsi ya kutafuti wanyama wakubwa kama Digidigi, nyani, mbega, nguruwe, pelepele na ndege, kwamba hutumia sauti zao, kuona kwa darubini, vinyesi vyao, alama za miguu pamoja na njia wanazopita. Halafu wajumbe walitembeza kuona na kujifunza kwa vitendo juu ya utafiti.

Mada ya sita ambayo iliandaliwa na Ndugu Selemani Hamadi (Bwana Miti wa Eneo) ilihusu matatizo yanayoonekana katika msitu wa Mlinga. Alianza kwa kuyataja matatizo makuu matatu ambayo ni sugu ndani ya msitu huu nayo ni: mioto ya mara kwa mara, uvunaji haramu na uwindaji wanyama.

Baada ya kuyataja matatizo aliendelea kueleza athari za matatizo hayo, kwamba moto husababisha uoto wa asili kutoweka na kuota mimea isiyo na manufaa, mfano mishigi. Pia moto huua wanyama wadogo wadogo. Moto huharibu rutuba ardhini, kuongezeka kwa panya

shambani na nyumbani, kuongezeka wanyama waharibifu mashambani kama nyani, na kusababisha viumbe kuhama kutoka sehemu moja mpaka nyingine.

Aliendelea kueleza madhara ya uvunaji haramu wa mbao kwamba miti muhimu hupotea au kutoweka, huharibu uoto wa asili na pia huua mimea iliyo jirani na pia husababisha maeneo wazi ndani ya msitu.

Uwindaji haramu ni hatari kwa kusababisha moto msituni, kuua wanyama, ukataji wa miti aina ya nguzo kufanyia mitego pia hiyo mitego huwa hatari kwa watu.

Mwisho mtaalamu huyo alipendekeza mambo ya kufanya ili kuepukana na matatizo haya. Alipendekeza kufanyike mikutano ya mara kwa mara na vitongoji vinavyopakana na misitu ya hifadhi hasa wakati na kabla ya kipindi cha hatari ya moto. Pia kuwe na doria za mara kwa mara kushirikiana na wanakamati, na kuhamasisha upandaji miti ya matunda, mbao, na kuni, pamoja na kuhamasisha kujishughulisha na kilimo misitu ili waweze kupata mahitaji yao karibu na makazi yao.

Baada ya mada ya mwisho, wajumbe walikaribishwa kuchangia hoja, maswali na kutoa mapendekezo yao juu ya somo hilo.

Wajumbe walikubaliana kwa kauli moja kwamba matatizo ya uharibifu wa mazingira ni makubwa na yanazidi kuongezeka kwa kasi ukilinganisha na hali ya hewa ya zamani. Walitaja sababu kuwa ni moto, shughuli za maendeleo, na uwindaji ndani ya msitu, pamoja na madhara ya kuzaana ambayo yanapelekea ongezeko kubwa la watu. Pia walikiri kutoweka kwa baadhi ya viumbe ndani ya msitu wa Mlinga kutokana na matumizi mabaya au yasiyoendeleu ya maliasili.

Hata hivyo wajumbe walikuwa na maswali kadhaa juu ya mada ya utafiti na wataalamu kwa ufasaha waliyajibu kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza lilihusu maeneo muhimu duniani ya bioanuwai mengine ukizingatia kwamba wataalamu wamesema hapa Usambara Mashariki ni la 24 kuwa na bioanuwai nyingi. Kwa kutumia ramani ya Dunia ambayo imeainishwa maeneo hayo mtaalamu Susannah Hall aliwaelimisha wajumbe na wakaelewa kwani eneo lao ni la 24 kidunia.

Swali la pili: Mjumbe alipenda kuelewa kwa nini utafiti unafanyika kwa has kwa wanyama na wadudu kama vile chura. Swali hili lilijibiwa na meneja mradi EUCAMP. Alianza kwa kueleza historia ya uumbaji wa mwanzo wa mimea na wanyama pamoja na kuwiana kwao. Aliongeza kwamba kiumbe kimoja kinamaana yake na huwa na uhusiano na kingine, na mara nyingi kuwepo kwa kiumbe fulani huashiria kuwepo kwa kingine. Na mara kimoja kikitoweka basi mfumo mzima hugeuka na mara nyingine huleta madhara makubwa kwa viumbe vingine. Mfano kama wanyama wakitoweka msituni basi wanyama kama simba, chui, fisi hula hata watu ambacho si kitendo cha kawaida. Mwisho alisema kama kungekuwa na upigaji kura kati ya binadamu na viumbe vingine kwamba yupi ni kero na hasitahiri kuwepo, basi binadamu kura ya kumuangamiza ingemuangukia kwa sababu ya vitendo vyake vya uharibifu.

Swali jingine: Mjumbe aliuliza: kutokana na kutokuwepo mawasiliano kati ya wanyama pori na wakulima, je watafiti hawawezi kugundua njia ya kuwasiliana nao ili wasiharibu mazao

yetu (wakulima)? Wataalamu Albert, Matiko, na Susannah walijibu kwa undani kama ifuatavyo:-

- Binadamu tumepewa akili na utashi wa kuvitawala viumbe, kwa hiyo tujitahidi kutumia uwezo huo kuwashinda wanyama bila kuleta madhara kwao.
- Mtaalamu wa pili alifurahishwa sana na swali hilo kuwa mjumbe ameweza kusema wanyama wa porini na sio waharibifu. Mwisho alipendekeza kwamba wananchi wapange matumizi bora ya ardhi kwa kujenga makazi kati ya mashamba na misitu.
- Mtaalamu wa tatu aliwaambia wajumbe kuwa kuwepo kwa wanyama waharibifu ni kutokana na matendo yetu mabaya ambayo yanaharibu mazingira na chakula kwa cha wanyama. Nao wakikosa mahitaji huja mashambani kwetu. Alimaliza kwa kupendekeza tuache vitendo vinavyosababisha moto msituni.

Swali la mwisho toka kwa wakulima lilikuwa ni hofu kuwa wanahisi kufichwa juu ya utafiti. Hisia ni kwamba watafiti wanatafuta madini na rupia ndani ya msitu Mlinga.

Jibu lilikuwa wao ni watafiti wa mimea na wanyama tu, na hawana utaalamu waowote juu ya madini. Waliwaomba wajumbe kuwa kama kuna madini basi serikali hutoa idhini ya kutafiti na endapo ikidhihirika kwamba madini yanafaida zaidi ya hifadhi ya misitu basi huo msitu hubadilishwa na kuitwa hifadhi ya madini. Baadae madini huchimbwa kwa manufaa ya nchi, kama ilivyotokea kwenye misitu ya huko Morogoro.

Kabla ya kufunga mafunzo kulikuwa na maswali dodoso yaliyoandaliwa na watafiti kama kipimo cha mafunzo yaliyotolewa.

*1) Ni sababu zipi zinazosababisha kupungua au kutoweka kwa misitu katika eneo unaloishi?*

Wajumbe walijibu nkupendekeza kama ifuatavyo:

Walijibu kwa kauli moja kwamba sababu kuu ni moto, kukosekana kwa elimu ya mazingira, uvunaji holela wa mbao na nguzo, uwindaji haramu na ongezeko la watu. Walipendekeza suluhisho la tatizo ni bwanamiti ashirikiane na kamati za mazingira, mipaka ya misitu na ya mashamba isafishwe, kuandaa mikakati ya kuielimisha jamii juu ya madhara ya uharibifu huo. Na mwisho walipendekeza mbiu zipingwe mara moto utokeapo na tahadhari zitolewe kipindi cha hatari ya mioto.

*2) Ni akina nani ambao hufanya uharibifu huo?*

Waharibifu wakuu wa misitu ni wananchi na zaidi ni wageni toka bara waliokuja kupasua mbao, pamoja na wawindaji haramu ndani ya misitu.

*3) Ni athari zipi ambazo zimetokea baada ya uharibifu wa miti kufanyika kwa muda mrefu?*

Walitaja athari kama ifuatavyo:

- kukosekana kwa mvua ya kutosha na kubadilika kwa misitu, mfano mvua za vuli hazitabiriki tena.
- wanyama na mimea muhimu wametoweka.
- vyanzo vya maji vimepungua au kukauka na kusababisha mito ya msimu badala ya ile ya kudumu.
- mila na desturi za hifadhi ya mazingira imepotea, mfano miiko mingi sasa haifuatwi.

4) *Wanyama wa aina gani wamepungua au kutoweka kwa sababu za uwindaji haramu na ukataji miti ovyo?*

Wafuatao ni wanyama ambao wanamazingira kwa kauli moja walikili kwamba wamepotea: simba, Chui, nyati, na waliopungua ni swala, digidigi, na ndege kama kanga.

5) *Unatoa ushauri gani ili kuzuia uharibifu huo usiendelee?*

-Walipendekeza kwamba wawindaji wote waorodheshwe, watambuliwe na hatimaye wapewe elimu ya mazingira ya wanyama na mimea.

-Njia mbadala ni kufuga wanyama kama vile kuku, mbuzi, pimbi, ng'ombe, n.k. Elimu na ushauri utolewe.

6) *Juhudi gani unazofanya katika kuhifadhi mazingira katika makazi unayoishi?*

Kila kijiji mjumbe alisimama na kueleza juhudi zinazofanyika na wote waliunga mkono kama ifuatavyo:

Misozwe:

- Wameandaa mikakati ya kuelimisha watu binafsi kuanzisha vitalu vya miti na kupanda miti.
- Wameandaa utaratibu wa kupanda miti ya asili kandokando ya mto upitao katika kijiji chao.
- Wiki ya Upandaji Miti kitaifa watapanda miti pembeni mwa barabara kuu iendayo Muheza kwa miti aina ya mijohoro.
- Kushirikiana na watu wa Magula kuhifadhi chanzo chao cha maji.

Magula:

- Wameweka mikakati ya kuhifadhi vyanzo vya maji ambavyo ndoyo uhai wa vijiji vya ukanda wa chini.
- Wameweka marufuku ya kukata miti au kulima kandokando ya mito au katika vyanzo vya maji.
- Wanaelimisha watu wasichome moto.

Magoroto-Mwembeni:

- Wamewahamasisha watu kuanzisha vitalu vya miti na kupanda miti mashambani pamoja na kwenye vyanzo vya maji na kandokando ya mito.

(NB. Hiki ni miongoni mwa vijiji anzilishi [pilot villages] katika shughuli za hifadhi misitu). Katika kuchangia juhudi za kuhifadhi misitu kujiji cha Misozwe na Magula waliazimia kuanzisha hifadhi ya misitu kwa kushirikiana kuhifadhi vyanzo vya maji na kuhifadhi kandokando ya mto.

7) *Ni sababu gani zinazokwamisha juhudi za upandaji miti kwenye makazi yako?*

Walitaja, upungufu wa miche, na iliyopo huuzwa kwa wengi wasio na vitalu. Walipendekeza mbegu zitolewe kwa watu wote, pia waelimisha kutafuta au kukusanya mbegu zao wenyewe.

Upungufu wa elimu na uhamasishaji juu ya upandaji miti na dhana nzima ya kilimo mseto (agroforestry).

8) *Unadhani ni kitu gani kitatokea misitu yote ikiharibiwa?*

Wajumbe walibashiri na kutaja kama ifuatavyo:

- kutatokea mmomonyoko wa ardhi na makorongo ya kutisha.
- kutatokea jangwa na ukosefu wa mvua.
- utoweka kwa malisho ya wanyama.
- upepo mkali na vimbunga vitatokea.
- kutaharibika majira na hali ya hewa itabadilika na kuwa mbaya.

9) *Je unaamini usemi huu: 'miti inaweza kuishi bila binadamu lakini mwanadamu hawezi kuishi bila miti'? Wewe unamtazamo gani?*

Wajumbe wate walikubali kwa kauli moja kwani kama binadamu hatakuwepo basi uharubifu utapungua na kubakia kama ilivyokuwa asili ya uoto na wanyama.

10) *Unadhani ni njia zipi zitumike ili kupata mahitaji kutoka msituni bila uharibifu?*

- Kamati za mazingira zitumike na zishirikishwe ili kulinda na kuelimisha jamii juu ya matumizi endelevu.
- Vibali vya mazao ya maliasili vianzie vijijini kwa kutumia kamati za mazingira.
- Kuwe na utaratibu maalum wa kuvuna mazao ya misitu.
- Kuanzisha na kuzilinda hifadhi za misitu za vijiji na kutumia katika matumizi endelevu.
- Kushirikishwa kwa wanakijiji katika kazi za utafiti pamoja na kupewa taarifa za mwisho za utafiti.
- Yote hayo yalipendekezwa na kupitishwa kwa kauli moja.

## **KUFUNGA**

Mgeni Rasmi Ndugu Matiko wambura (Meneja Mradi, EUCAMP) aliombwa kusema machache juu ya mafunzo na mwisho aliombwa kufunga mafunzo ya elimu ya mazingira.

Alianza kwa kutoa shukurani zake za dhati kwa watafiti (Frontier-Tanzania) kwa kuandaa na kutekeleza mpango wake wa elimu ya Mazingira kwa jamii inayozunguka msitu unaotafitiwa, pamoja na kuwajulisha matokeo ya utafiti. Pia alitoa shukurani zake kwa wanakamati za mazingira wa Misozwe, Magula na Miembeni, pamoja na viongozi wao kwa kuhudhuria mafunzo hayo.

Alikiri kwamba mafunzo yamewafikia walengwa kutokana na michango yao katika mada zote na madhumuni yake pia yamedhihirika. Mfano:

- Wameweza kukutana na kufahamiana wanakamati za mazingira.
- Kueleweshwa juu ya mbinu za utafiti kwa vitendo na kuona matokeo yake.
- Pia wameweza kujua vyanzo vya uharibifu wa mazingira, madhara yake na mbinu za kukabiliana na matatizo hayo.

Alisisitiza kwamba matokeo ya utafiti ni muhimu sana katika kupanga na kutekeleza sera za ushirikishwaji wa jamii katika misitu ya hifadhi za taifa na za vijiji (Joint Forest Management programme, JFM). Hii ndio sera ya taifa na idara ya misitu ndio itasimamia katika kuwezesha wanavijiji kumiliki misitu yao, kuanzia ngazi ya mtu binafsi, familia hadi kijiji. Pia miti ya asili iliyopo ndani ya mashamba kumilikiwa na wakulima na kuitumia katika matumizi endelevu chini ya usimamizimwa wataalamu wa misitu.

Alikiri kwamba chanzo kikubwa cha uharibifu wa misitu ni elimu duni ya mazingira ambayo ni muhimu sana katika kuhifadhi misitu. Lakini aliwafariji kwa kuwaeleza kuwa msitu huo wa Mlinga upo ndani ya mpango kabambe wa kuishirikisha jamii katika kuhifadhi misitu ya taifa (JFM). Na aliwaomba wajumbe wawe mabalozi katika kufikisha ujumbe huu. Pia aliwaomba kwamba wayatumie madaraka waliyopewa bila woga wala unafiki kama vile kuwaficha waharifu wa mazingira.

Aliwaambia wajumbe kwamba mtazamo wa ofisi ya Hifadhi Mkoa “tutashirikiana katika kuhifadhi maeneo yaliyopo ndani ya vijiji, kama vile vyanzo vya maji, misitu ya vijiji, n.k. Pamoja na kusaidia vijiji katika kuweka mipango ya utekelezaji wa hifadhiya mazingira.

Mwisho alishukuru tena watafiti kwa kuweka na kutekeleza mpango wa elimu ya mazingira. Aliomba taasisi nyingine za kiserikali na zisizo za kiserikali kuiga mfano mzuri huo. Kikao kilifungwa mnamo saa 9:45 jioni.

Photograph of Misozwe Environmental Committee with Frontier and EUCAMP staff.



### 7.3: Mlinga Womens Group Meeting Agenda (Kiswahili & English)

Wajumbe waliohudhulia

No.	JINA	CHEO
1	Susannah Hall	Kiongozi wa utafiti, Frontier-Tanzania
2	Albert Ntemi	Kiongozi wa utafiti Hifadhi Mimitu, EUCAMP
3	Hanifa Juma	Mwalimu, Misozwe Primary School
4	Bibie Selemani	Mwalimu, Misozwe Primary School
5	Mwanaidi Shabani	Mwalimu, Misozwe Primary School
6	Flora Mbwana	Mwalimu, Misozwe Primary School
7	Monica Sekimweri	Mwalimu, Misozwe Primary School
8	Ester Majama	Mwana kikundi
9	Zaina Ali	Mwana kikundi
10	Zaina Salimu	Mwana kikundi
11	Pili Hamza	Mwana kikundi
12	Mary Msumi	Mwana kikundi
13	Rhoda Makuo	Mwana kikundi
14	Mariam Mngazija	Mwana kikundi
15	Salima Mohamed	Mwana kikundi
16	Pili Amiri	Mwana kikundi
17	Mary Mhina	Mwana kikundi
18	Fatuma Mgallawe	Mwana kikundi
19	Agatha Selevesta	Mwana kikundi
20	Tarendane Aseri	Mwana kikundi
21	Joyce Tupa	Mwana kikundi
22	Monika Endward	Mwana kikundi
23	Joyce Nyangue	Mwana kikundi
24	Rhoda Lumuliko	Mwana kikundi
25	Mary Mathayo	Mwana kikundi
26	Gces Yakobo	Mwana kikundi
27	Stera Wares	Mwana kikundi
28	Joyce Semakome	Katibu kikundi
29	Selemani Hamadi	Bwana Miti, Misozwe

#### Kamati za wanawake – Ratiba (Kiswahili)

- 9.00 am** Kukaribisha wageni na chai (Selemani Hamadi)
- 9.30 am** Utangulizi na kujitambulisha (Susannah Hall)
- 9.45 am** Mimitu ya Usambara Mashariki (Albert Ntemi)
- 10.00 am** Umuhimu wa utafiti (Albert Ntemi)
- 10.15 am** Vitu tunanyotafiti (Albert Ntemi)
- 10.30 am** Mapumziko mafupi na chai
- 11.00 am** Matatizo ya mimitu wa Hifadhi wa Mlinga (Selemani Hamadi)
- 11.30 am** Majadiliano / Majiko sanifu
- 12.00 pm** Maswali machache kukota Frontier-Tanzania
- 12.30 pm** Kuona 'specimens' (Frontier Tanzania)
- 1.00 pm** Chakula na kufunga kikao

**Women's Group Meeting – Timetable (English)**

- 9.00 am** Welcome, tea and registration (sign visitors book & complete form) (Local Catchment Officer)
- 9.30 am** Introduction (Susannah Hall)
- 9.45 am** East Usambara mountains Forests (Albert Ntemi)
- 10.00 am** Importance of biodiversity research (Albert Ntemi)
- 10.15 am** What are we doing in the forest? (Albert Ntemi)
- 10.30 am** Tea break
- 11.00 am** Problems of Mlinga FR (Local Catchment Officer)
- 11.30 am** Discussion about new improved stoves
- 12.00 pm** Questions to Frontier-Tz and EUBS
- 12.30 pm** Specimen viewing (Frontier Tanzania)
- 1.00 pm** Lunch and closing

**Makiko sanifu**

1. Je majiko sanifu yamewasaidiaje katika uhifadhi wa misitu na mazingira?  
*How have the improved stoves assisted you in forest conservation?*
2. Elimu hii ya Majiko sanifu, je mmeienezaje kwa waki na mama wengine katika kijiji chenu?  
*To what extent has the improved stove knowledge/training spread amongst other women?*
3. Aina ipi ya majiko ni bora zaidi?  
*Which is the best new improved stove? Why?*
4. Je mnamalengo yapi mengine ya kuhifadhi misitu zaidi ya huo wa majiko sanifu?  
*Is there any other environmental conservation measures you are planning to start apart from the improved stove?*

## **7.4: Lesson Plans for School visits**

### **7.4.1: Catchment Officer Talk**

#### **(a) Suggested Content (English)**

##### **Goal**

To increase the children's interest, respect and sense of responsibility for local Forest Reserves.

##### **Key questions to address during visits:**

- What is a Forest Reserve?
- Why are they important?
- Who do they belong to?
- Who looks after them?
- Where would we be without them?

##### **Catchment Officer (CO) Talk:**

###### **What is a CO?**

I work with local village people to help them make use of Forest Reserves in a way that doesn't damage them. There are people like me in charge of all of the Forest Reserves in the E. Usambaras (see map). The Government has created these jobs because they know how important the forests are to the local people.

###### **What is a Forest Reserve?**

These are important areas of land because they contain

- the water source for the surrounding low-lying villages
- a fuelwood source

The Government knows how important these areas are for the local villages and so it has protected them.

###### **What does a CO do?**

I encourage villagers who live close to Forest Reserves to look after them properly. I talk to village Environmental Committees and other groups to improve the way we use our forests.

The FRs are a 'resource' - which means that they are ours to use, but we must use them carefully if we are to enjoy them for years to come.

###### **Some of the things I am involved with are:**

1. **Creating tree nurseries**, like the one in the school. These are important to stop people illegally cutting down trees in the FRs to use for building materials. Tree nurseries are also good as they teach us how to grow and care for our trees which we can use or sell to raise money for the school.
2. **Creating wild vegetable nurseries** in villages. This is to stop people illegally harvesting wild plants from the forests and so that they have nice things to eat and to sell in town.
3. **Teaching people how to light safe fires** that do not burn down the forest by mistake. People must tell the village Environmental Committee before they light fires, otherwise they will be fined. I teach them how to clear vegetation around their shambas and keep watch on fires so that they do not spread beyond their fields and into the FR.

4. **Trying to stop illegal hunting.** Any form of hunting or harvesting (except for collecting dead wood) is against the law in Tanzania in FRs. People caught hunting are punished by the Government. Hunters often start fires by mistake that burn off large areas of forest. It is a real problem as the forest burns very quickly in the dry weather. Lots of plants and animals die in the fires and it destroys the reserve.
5. **Improving cooking stoves.** We all use a lot of firewood to cook our food. I am helping to promote a new clay stove that uses much less firewood than an open fire. This is great as it means less wood needs to be gathered each day and it means less damage to our FRs. It is a stove that we can make in our villages. Do you have one at home?
6. **Encouraging beekeeping groups** in villages. Kwatango, for example, have over 40 beehives and the village shares the honey and sells any they have left over. This is good because everyone likes honey and it stops people going into the FR and illegally harvesting wild honey.
7. **Encouraging fishkeeping** in pools to help stop people illegally hunting in the forest. This has been possible in Magoroto where there is more rain.

### **What are the Frontier people doing?**

They have come to look for all the special plants and animals that we have in our Forest Reserves. They are writing down all of the plants and animal types that they find in a list. There are many unusual types of animals, trees and plants here that aren't found anywhere else in the world. That makes these reserves very special (see endemics poster).

### **(b) Hifadhi ya Misitu, Siku Ufundishaji Shule ya Msingi (Kiswahili)**

#### **Lengo**

Kuongeza kiwango cha hisia kwa wapafunzi kupenda, kuheshimu na hisia za wajibikaji wa wanafunzi juu ya mazingira hasa misitu ya hifadhi iliyo karibu nao.

#### **Maswali ya msingi**

(Wakati wa kufundisha)

Msitu wa hifadhi ni nini?

Umulu mu wake ni nini?

Msitu wa hifadhi ni uali ya nani?

Nani anawajibika kwatunazi?

Bila ya misitu tungekuwa wapi?

#### **Nukuu kutoka kwa afisa misitu afisa misitu ni nani?**

“Ninafanya kazi na wananchi ili kuwawezesha kutumia/kunufaika na misitu ya hifadhi kwa njia ambazo hazitaleta uharibifu”

“Wapo watendaji wengine kama yeye katika misitu yote ya Usambara mashariki (angalia ramane). Serikali iliamzisha usima mizi huu kwa vile inafahamu umuhimu wa misitu kwa wanachi wake.

#### **Misitu ya hifadhi ni nini?**

Haya ni maeneo muhimu kwa sababu.

(i) Ni maeneo ya vyanao vya maji kwa maeneo yaliya karibu.

(ii) Kuni kwa ajili ya nishati hupapti kana humo. Serikali inafahamu umuhimu wa maeneo haya kwa wali wakew nelio maana imeamaa kuyatenga na kuyali nza.

**Kazi ya afisa misitu ni nini?**

Kuwahamasisha wananchi waishio karibu na misitu tu ya hifadhi (mfano msitu wa Mlinga) kuulinda na kuutunza kwa dhati, husaidiana na kamati za mazizigira za vijiji na vikundi vingine kuwaelimisha wananchi juu ya matumizi mazuri ya misitu yetu.

Misitu ya hifadhi ni “maliya asili” tui tumiayo, lakini hatuna budi kuitumia kwa uangalifu mkubwa ili tuweze kuifaidi kwa miaka mingi.

**Kazi nyingine ambazo afisa misitu anazifa nya**

1. Uanzishaji wa vitalu vya miti, kama kitalu chenu cha miti. Hii ni moja ya njia muhimu ya kupunguza ukatati miti ovyo katika misitu ya hifadhi kwa ajili ya ujenzi. Vitalu vya miti ni muhimu kwa sababu tunajifunza jinsi ya kuotesha mbegi, za miti, utunzaji wa miti ambayo baa daye tunaitumia, pamoja na kuuza ili kupata fedha kwa ajili ya shule yetu.
2. Uanzishaji wa bustani za mboga, katika vijiji. Ulimaji wa mboga moboa ni ili kupunguza kutegemea uvunaji wa majani ya mboga kutoka msituni. Badala yake mboga mboga hizo tunatu mia na nyingine kuuza.
3. Kuelekeza matumizi mazuri ya moto, ambago hauwezi kuleta madhara kwenye misitu pale inapotumika. Wananchi wanao wajibu wa kutoa taarifa kwa kamati za mazingira za vijiji kabla ya kuchoma moto katika mash a yao, vinginevyo hatua za kisheria zitachuku liwa dhida yao. Vilevile afisa misitu anaelekeza narina ya kusafisha shamba kabla ya kucho ma moto na jinsi ya kuchunga moto usieriee katika misitio ya hifadhi moto unapotumika mashambani.
4. Kuzuia uwindaji haramu. Aina yoyote ya uwindaji (ou uvunaji wa mali asili (isipokuwa kuokota kuni kavu) ni kinyume na sheria za misitu za Tanzania. Mtu yeyote anayekamatwa kwa mako sa hayo anahukumiwa kulingana na sheria za nchi. Wawindaji mana nyingi wamekuwa ndio charizo cha moto misituni kwa vile huchoma moto kwa nia ya kuwaua wanyama, ambapo baadaye hua cha moto huo kuendelea kuwa na kuchoma msitu. Msitu unaungua kwa kwa mfano kij haraka sana hasa nyakati za ukame (kiangazi) na kusababisha mali hai nyingi hasa wanyama na mimea adimu kuungua moto.
5. Utengenezaji na utumiaji majiko sanifu. Sisi wote lazima tukubali kwamba tunatumia kuni nyingi sana kupikia vyakula vyetu. Afisa misitu husaidai wananchi kutumia majiko yana yotengenezwa kwa udongo wa mfnyanzi yanayo tumia kuni kidogo sana kulinganisha na jiko la mafiga matatu. Hii ni hatua kubwa sana ya kuokoa misitu yetu. Ni majiko ambayo kila mtu anaweza kutengenezea. Je kila mmoja wenu wanalo nyumbani kwenu?
6. Kuhimiza ufugaji wa nyuki ki vikundi katika vijiji, kwa mfano kijiji cha kwatango wana zaidi ya mizinga ya nyuki 40, wanavikundi hugawana asali na ziada huuza na kujipatia fedha. Huu ni mfano mzuri wa kuigwa kwa vile utasaidia kuondoa tatizo la uwindaji asali kutoka msituni isivyo halali.
7. Kuhimiza ufugaji wa samaki kwa kuchimba mabwawa madogo madogo ya kifamilia, hii itasa iolia kuondoa tatizo la uwindaji haramu kwa ajili ya kitoweo. Ufugaji wa samaki umeanza kuenea sana katika eneo la Magoroto ambago hupatikana maji kwa urahisi.
8. Watafiti kutoka (Frontier) wamekuja kufanya nini? Watafiti hawa wamekuja kutafiti na kuchunguza aina mbali mbali aalum za wanyama na mimea zipatikanazo kwenye msitu

wa Mlinga. Wamekuwa wakiorodhesha wanyama na mimea ya pekee ipatikanayo katika misitu ya hifadhi ya Usambara mashariki. Baadhi ya aina za mimea na wanyama wana patikana hapa tu na hawapatikani sehemu nyingine duniani (angalia bango la viumbe adimu). Hii inafanya viumbe hivi viwe ni viumbe vya pekee duniani.

#### 7.4.2: Environmental Trail

##### **(a) Environmental Trail Lesson (English)**

- Emphasis:** 1. Science  
2. Geography (Extension/follow-up lesson)
- Age group:** 6+ **Lesson length:** 30 min
- Aim :** To increase awareness of the “immediate” environment.
- Objectives:** 1. To explore biodiversity in school grounds, e.g. (signs of) animals, plants, trees, insects/butterflies, through observation of the grounds.  
2. To be able to geographically represent features of the environment.
- Resources:** Plain paper  
Wax crayons  
Writing pencils  
*Binoculars, butterfly sweepnets, magnifying glasses, specimen pots, compasses, sound-recording/playing equipment\**  
(\*non-essential, suitable for lesson extension ideas. May be safety issue with magnifying glasses in dry grass)

##### **Methodology:**

1. Choose a location in the school grounds and ask the children what they understand the word “environment” to mean (this can be done as an introduction or as a reminder at the end of the lesson if children are already familiar with the word). (5 min)
2. After establishing that it is “the world around us” (or other similar definition), say that we are looking for living things within the school environment and/or signs of things that have been there. Will need to consider how to go about this without damaging grounds etc. (5 min)
3. Distribute drawing apparatus and show any other resources.
4. Split into smaller groups to look for signs, such as bird nests, bark/leaf rubbings, flowers, birds/butterflies/insects. Find as much as possible within 20 min.
5. Reassemble to discuss what was found. Look at good examples. Comment on findings.

##### **Lesson Extension:**

6. After returning to classroom, draw a map of the school and where living things were found. This can be extended further for more able/older children by increasing the area to include village, rivers, Forest Reserve, catchment areas.
7. A sound environmental trail, listening for evidence, recording and identifying sounds.
8. Use more technical equipment. Measuring trees, collecting insects etc.
9. Introduce more technical scientific terms to the environmental trail, e.g. invertebrates/vertebrates.
10. Change the emphasis of the trail from natural signs to looking for signs of man’s uses of/impacts on the environment. Examples of impact may include: burning, cultivation,

water taps, brick furnaces, grazing, medicinal uses of trees. This could lead onto discussions on environmental concerns back in the classroom.

**Evaluation:**

Evaluate how the lesson went by using feedback from children, general comprehension of the term “environment” and the interpretation of children’s work sheets.

**(b) Uchunguzi wa Mazingira (Kiswahili)**

**Mkazo:** 1. Sayansi/Jiografia

2. Jiografia (Upanuzi wa somo)

**Umri drs:** 6+

**Muda dk:** 30

**Kusudi:** Kuongeza ufahamu wa mazingira ya karibu sana na wanafunzi wanamoishi.

**Lengo:** 1. Kuchunguza bioanuwai katika maeneo ya shule mf (alama za) wanyama, mimea, miti, wadudu, vipepeo kwa kuangalia adhini.

2. Kuwa na uwezo wa kuviwakilisha kijiografia vitu vilivyo kwenye mazingira.

**Vifaa:** Karatasi isiyo na mistari

‘Wax crayons’

Penseli

Kionambali, chandarua za vipepeo, vioo/miwani ya kukuzia, chombo chenye vitu vya mazingira, compasses, vinasauti\*

(\*si lazima, vyafaa kwa mwendelezo/upanuzi wa somo)

**Njia:**

1. Baada ya kuchagua enco katika mazingira ya shule wanafunzi wataulizwa wanaelewa nini maana ya neno ‘mazingira’. (Yaweza kufanyika kama utangulizi wasono au mwisho kuona kama wanafunzi wameielewa maana) dk 5.

2. Baada ya kueleweka kuwa ni “eneo linalotuzunguka” (au ufafanuzi unaofanaua na huo), sema kuwa tunatafuta viumbe hai katika mazingira ya shule na/au alama ya vitu vilivyokuwepo. Ni muhimu kuangalia ufanikishaji wa zoezi hili pasipo kuharibu mazingira. dk 5.

3. Gawa vifaa vya kuchorea na onyesha nyenzo nyingine yoyote.

4. Wagawe wanafunzi katika makundi madogomadogo, katika kuangalia alama, kama viota vya ndege, majani/magome ya miti, maua ndege, vipepeo, wadudu. Tafuta vingi iwezekauavyo kwa dk 20.

5. Kusanyikeni tena kujadili vilivyopatikana. Toa maoni juu ya matokeo.

**Nyongeza/upanuzi wa somo:**

6. Darasani, chora ramaniya shule, na wapi viumbe hai vimepatikana. Kwa wanafunzi wakubwa panua hadi kuonyesha kijiji, mito, na msitu wa hifadhi.

7. Sikiliza sauti, rekodi na tambua sauti.

8. Tumia vifaa vya kitaalamu zaidi. Kupima miti, kukusanya wadudu n.k.

9. Ingiza maneno ya kitaalamu zaidi katika uchunguzi wa Mazingira mf. Viumbe wasio na uti wa mgongo/wenye uti wa mgongo.

10. Badili msisitizo wa uchunguzi toka alama za vitu asilia kuangalia alama za matumizi ya binadamu/madhara katika mazingira. Mifano ya madhara inaweza kujumuisha uhomaji moto, ulimaji, mabomba ya maji, matanulu ya matofali, ulishaji mifugo, matumizi ya miti kwa dawa. Hii inaweza kupelekea mjadala juu ya uwajibikaji katika mazingira mrudipo darasani.

**Tathmini:**

Kutoka katika mawazo ya wanafunzi na uelewa wa neno ‘mazingira’ na kutokana na kazi za wanafunzi. Pia maoni ya walimu na yako binafsi.

**7.4.3: What’s in the bag?**

**(a) What’s in the Bag Lesson (English)**

**Emphasis:** 1. Science  
2. Language

**Age group:** 6+

**Lesson length:** 30 min

**Aim:** To increase awareness of the variety of living things found in the Forest Reserve.

**Objectives:** 1. To aid recognition of living things.  
2. To increase use of descriptive language.

**Resources:** Cloth drawstring bags (at least 2 per group of 10 children).  
Assorted objects found in forest, for example:  
Shells, seeds/seedpods, feathers, birds’ nests, fur, bark, dry grass/fresh grass (reference to fire risk), teak leaves (reference to border marker trees)  
Cassette player and blackboard\*  
(\*Required for lesson extension idea)

**Methodology:**

1. Sit the children down into groups of approximately 10 in a circle with one teacher/Kiswahili speaker per group and other helpers.
2. Explain that there are natural things from the Forest Reserve inside the bag.
3. Pass the bag around and, without them looking inside, ask the children to put a hand into the bag to carefully feel what’s inside and for them to use one word to describe how it feels. Each must be a different word from the previous one. They must not say what is in the bag at this stage.
4. After the last child has had a go, ask each child in turn what they think it might be. Reveal the object to show if they were right and pass it round again if required.
5. Repeat this process until the end of the session (about 5 objects). Exchange bags with other groups as required.

**Lesson extension:**

6. Play sounds on a tape so the children draw what animals they can hear within a 5 min (or given) period. Then go through the tape again commenting when sounds are heard (writing/drawing on board to illustrate).

**Evaluation:**

The children's ability to guess the objects correctly and skill improvement.

**(b) Kuhisi Kuna Nini Ndani ya Mfuko? (Kiswahili)**

**Mkazo:** Sayansi/Lugha

**Umri drs:** 6+

8) Ni njia zipi zitumike ilikupata mahitaji kutoka misituni bila kuharibu?

- Hili kama swali la mwisho wanakamati walichangia kama ifuatavyo.
- Ushirikishaji wananachi.
- Kuwa na wataalam kabla ya kutumia miti.
- Mikakati ya kwana kwa utalam.
- Panda miti kata miti.
- Kuimarisha doria ndogondogo.
- Doria za mara kwa mara.

Mwisho wanakamati walihitimisha mkutano kwa kutoa shukrani na kuelezea mambo mazuri waliyojifunza kuhusu mazingira. Shukrani kwa watoa maada na waliomba semina hizi ziwe mara kwa mara na kuahidi kwa dhati kwamba watakwenda kuyafanyia kazi huko waendako.

Saa 8.25 ilikuwa ndio mwisho wa kikao. Mwenyekiti wa kikao alitoa nasaa zake na kuwashukuru wanakamati kwa mwitikio wao wa kikao.

## MAELEZO YA MAJADILIANO

### UTANGULIZI KWA FRONTIER NA WATAFITI WA BAYOANUWAI WA USAMBARA MASHARIKI (EUBS)

*Sam Staddon (Kiongozi wa Utafiti, Frontier-Tanzania)*

Karibuni katika kambi ya utafiti Usambara Mashariki. Jina langu ni Sam Staddon. Mimi ni kiongozi wa utafiti. Ninafanya kazi na Frontier-Tanzania. Frontier-Tanzania ni ushirikiano baina ya umoja wa utafiti wa mazingira na chuo kikuu cha Dar-es-Salaam. Frontier-Tanzania wamepewa mkataba na Programu ya uendelezaji wa misitu ya Usambara Mashariki (EUCAMP) kutafiti viumbe adimu katika misitu yote ya hifadhi.

Kikundi cha watafiti katika msitu wa hifadhi Bombo Mashariki 1 na 2 (Kilimandege na Kilimamwarabu) kinajumuisha wafanyakazi wawili wa misitu; Albert Ntemi na bwanamiti Ntogolela. Tuna viongozi watano wa Frontier, wasaidizi watananzania watano na wasaidizi wazungu kumi na tatu (kutoka Ulaya). Tunafanya kazi hapa kwa wiki kumi.

Leo, tumewakaribisha hapa kubadilishana mawazo kuhusu bayoanuwai (mimea na wanyama) na utunzaji wa misitu katika milima ya Usambara Mashariki hasa misitu ya hifadhi Bombo Mashariki 1 na 2 (Kilimandege na Kilimamwarabu). Utafiti huu ulianza mwaka 1994 na umekuwa na matokeo mazuri sana kwa kufanikiwa kupata mimea na wanyama ambao walikuwa hawajulikani na pia kuongeza orodha ya mimea na wanyama. Misitu 14 imeshafanyiwa utafiti kama huu katika misitu ya Usambara Mashariki:

Kambai	Kwamngumi (Kwamtili)
Longuza	Mlungui (karibu na Bamba)
Kwamarimba	Mtai (karibu na Maramba)
Bamba	Magoroto
Manga (Lanzoni)	Amani
Segoma	Nilo (karibu na Kwemkole, Kizara na Kilanga Ngua)
Semdoe	Mlinga (karibu na Mesozwe)

Lengo la utafiti wa viumbe adimu katika milima ya Usambara Mashariki:

- Kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu thamani ya viumbe adimu ndani ya misitu katika kuboresha mpango wa utunzaji misitu na ufuatiliaji wa muda mrefu.
- Kutafiti mimea na wanyama adimu ndani ya misitu ya hifadhi.
- Kusaidia mpango wa utunzaji wa baadaye wa misitu.
- Kutoa mafunzo ya utafiti kwa Mabwana na mabibi miti.
- Kutoa ripoti ya kila msitu ikionyesha matokeo ya utafiti na ushauri wa utunzaji wa misitu kwa matumizi endelevu.
- Kuchunguza uharibifi wa misitu.

Mafanikio ya Utafiti:

- Umefanikiwa kutafiti misitu 12 na huu ni wa 13.
- Mimea mingi imeweza kujulikana kwa wanamimea ambayo ilikuwa haifahamiki hapo nyuma.
- Wanyama wadogo wadogo wengi wamejulikana kutoka na utafiti huu.
- Utafiti huu umeweza kuelimisha njia mbali mbali za utafiti kwa mabwana na mabibi miti katika Mradi wa hifadhi Misitu Usambara Mashariki.
- Watafiti mbali mbali wamevutiwa na kufaidika na utafiti huu.
- Kujulikana zaidi ulimwenguni umhimu wa misitu hii ya Usambara Mashariki kupitia utafiti huu.

## UTANGULIZI KUHUSU SAFU YA MILIMA YA UKANDA WA MASHIRIKI

Albert Ntemi Sallu, Mwanabayoanuwai, EUCAMP

### Je unaifahamu safu ya Milima ya Ukanda wa Mashiriki?

Safu ya Milima hii imeishia mwambao wa Pwani ya Kaskazini-Mashiriki, kutokea Kusini Magharibi mwa Tanzania, imeumbwa na milima tisa iliyotengana kuanzia Kusini mwa nchi ya Kenya kupitia Tanzania ikifanya umbo kama la mwezi mchanga uliochomoza na ndiyo maana ya jina la “Safu Ya Milima Ya Ukanda wa Mashiriki” (The Eastern Arc Mountains).

### Safu ya Milima ya Ukanda wa Mashiriki ni ipi?

Angalia ramani: Taita Hills (Kenya), Pare Kaskazini na Kusini, Usambara Mashiriki na Magharibi, Nguu, Nguru, Ukaguru, Robeho, Uluguru, Udzungwa, Mahenge

### Kipi kilisababisha milima hii ionekane kama ilivyo sasa?

Inasemekana kwamba misitu mikubwa ya mvua nyingi ya Afrika Magharibi ilikuwa imesambaa bara zima la Afrika. Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, miaka milioni kumi iliyopita, misitu hii ya Mashariki ilijitenga kutoka misitu ya Afrika Magharibi. Kutokana na ukame na shughuli za maendeleo za binadamu kuongezeka milima hii imekuwa ikitengana kutoka safu moja baada ya nyingine na kuonekana kama visiwa (vilivyozungukwa na mbuga za majani, vichaka, mashamba, makazi ya watu nk.).

### Nini umuhimu wa misitu iliyopo katika milima hii?

1. Kuwa inahifadhi vyanzo vya maji
2. Watu wanaoshi maeneo haya wanapata mahitaji yao kutoka katika misitu hii kama vile maji, kuni, mkaa, dawa, nguzo, za kujengea na mbao kwa ajili ya matumizi mbalimbali
3. Pia misitu hii inatengeneza mandhari katika maeneo husika na imekuwa kivutio kikubwa kwa watalii.
4. Zaidi ya hayo, misitu hii ina umuhimu katika kuhifadhi ardhi na kurekebisha hali ya hewa na pia ina mchango mkubwa sana katika kuwepo kwa mvua zinazonyesha katika maeneo hayo. Kwa hiyo milima hii ni uti wa mgongo wa Taifa letu na urithi wa vizazi vijavyo. Na kiulimwengu ni ya 24 kuwa na Bayoanuwai nyingi (aina mbalimbali ya viumbe hai).

### Je unafahamu kwamba misitu hii inakabiliwa na hatari ya kutoweka?

Cha ajabu ni kwamba misitu iliyoko katika milima hii hukatwa sana kwa ajili ya mbao na matumizi mengine pamoja na kuchomwa moto ovyo. Ingawa kuna udhibiti lakini uvunaji haramu wa mbao bado ni tatizo sugu.

### Nini athari (madhara) za kuharibu misitu hii?

Baadhi ya madhara ya uharibifu wa miti, hutokea baada ya muda mfupi na mengine huchukua muda mrefu kujitokeza. Athari hizo ni pamoja na:

1. Mmomonyoko wa udongo na maporomoko ya ardhi
2. Ukame
3. Kutokea kwa mafuriko
4. Kukauka kwa vyanzo vya maji
5. Kutoweka kwa aina fulani ya miti
6. Kutoweka kwa aina fulani za viumbe hai kwa mfano wanyama, wadudu, ndege, mimea, nk.

7. Mabadiliko ya hali ya hewa, mfano kuongezeka kwa joto duniani, gesi ya hatari kwa binadamu mfano CO, CO<sub>2</sub>.

Kuna juhudi zozote zinazofanyika katika kuhifadhi misitu iliyoko kwenye Milima ya Ukanda wa Mashariki?

Kwa vile umuhimu wa Safu ya Milima ya Ukanda wa Mashariki unaeleweka vema kwa wanabiolojia na watafiti tu, tumeona kuna haja kubwa ya kueleemisha jamii nzima ya Tanzania ifahamu kinachoendelea kuhusu Bayoanuwai (Biodiversity- Maisha ni Kuwiana Baina ya Viumbe, Binadamu na Mazingira yao) iliyo hazina kubwa kwetu. Elimu ya mazingira imeanza kutolewa kwa wananchi wanaoishi katika milima hii, kuhusu madhara ya kuharibu mazingira. Serikali na mashrika yasiyo ya kiserikali yameanzisha juhudi za kuishirikisha jamii inayoishi au kupakana na maeneo ya misitu katika kuhifadhi misitu. Juhudi hizo ni pamoja na kuwahamasisha wananchi kupanda miti katika mashamba yao kwa ajili ya matumizi yao. Pia juhudi zinafanywa kuwaelimisha wakulima juu ya kilimo misitu (kilimo mseto).

## **UTANGULIZI KUHUSU MISITU YA USAMBARA MASHARIKI**

Albert Ntemi Sallu, *Mwanabayoanuwai*, EUCAMP

Misitu ya Usambara Mashariki ni Miongoni mwa Misitu ya mvua ya ukanda wa mashariki (Eastern Arc Mountains) na ni kati ya Misitu ya hifadhi yenye thamani katika bara la Africa. Kuna baadhi ya mimea na wanyama ambao wanapatikana tu katika misitu ya Usambara Mashariki. Misitu hii ni muhimu katika utoaji wa maji kwa wananchi wa Tanga mjini na watu wote wanaoishi kando kando ya Milima hii.

*Mpango wa utunzaji wa Misitu ya Usambara Mashariki umefanikiwa Kuanzisha Hifadhi ya Mazingira Asili ya Amani yenye malengo ya:*

- Kuhifadhi Vyanzo vya maji,
- Kuanzisha na kutunza misitu ya hifadhi.

Kuendeleza faida za misitu kwa wanavijiji.

Utafiti katika Misitu ya Usambara Mashariki ulianza Miaka ya 1890 hasa katika ukusanyaji wa Mimea. 1928 utafiti wa vyura ulifanyika, na kati ya 1930 kazi ya utafiti wa ndege ilianza. Tangu utafiti huo wa awali, utafiti wa bayolojia katika milima hii umezidi kuongezeka.

Wananchi wa waeneo haya wanategemea misitu hii kwa mahitaji yao mengi ya kila siku, kwa mfano; Kuni, Maji, Mboga, Matunda, Dawa, Majengo, Mvua, Uyoga, hewa nzuri, n.k. Ingawa umuhimu huu wa Misitu hii unafahamika kwa wananchi wa milima hii ambao ndio watumiaji wakuu, bado uharibifu wa misitu unatokea mara kwa mara ambao unahatarisha misitu. Uharibifu kama, uchomaji moto, uvunaji haramu wa mbao, uwindaji, ukataji, majengo na fito, ulimaji ndani ya misitu na mwingine mwingi, ni hatari kwa misitu hii kwa hapo baadae kama hautakomeshwa mapema.

Wananchi wanatakiwa kujivunia na utajiri walio nao wa misitu hii na waitunze kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo kwa matumizi endelevu. Maeneo mangi hapa Tanzania hayana Milima na misitu minene na mizuri kama hii. Ukame ni tatizo katika maeneo hayo hivyo

isingekuwa vizuri kutoweka yote. Tushirikiane kuitunza misitu ya Usambara Mashariki kwa nguvu zote.

## **MISITU NI UHAI!**

### **VITU TUVYOTAFITI NDANI YA MISITU YA HIFADHI**

Amiri Saidi, Msaidizi wa Utafiti na Albert Ntemi Sallu

Katika misitu ya hifadhi ya Usambara Mashariki, tunatafiti viumbe hai ndani ya maeneo yote ya misitu ya asili, kwa mfano:

#### *Wanyama:*

- wanyama wadogowadogo kama panya, popo, vyura, nyoka, mijusi, ndege, wadudu kama vipepeo, konokono, jongoo

#### *Mimea:*

- Kutambua majina ya miti ya kitaalamu na ya kienyeji
- kukusanya mimea na kuipeleka sehemu mbalimbali ulimwenguni kwa ajili ya kutambulika zaidi na kuhifadhiwa kwa matumizi ya baadaye.

#### **Kuchunguza uharibifu wa Misitu:**

Hapa tunapita sehemu zote za msitu na kuangalia uharibifu uliofanywa na watu.

- Uharibifu kama ukataji miti, fito, na nguzo.
- Uchanaji mbao
- Uwindaji haramu wa wanyama
- Uchomaji moto ovyo

Sampuli zilizokusanywa za mimea na wanyama kwa kutumia njia za kitaalamu. Sampuli hupelekwa kwa wataalama Dar-es-Salaam, Uingereza, Zimbabwe, Marekani na Ujerumani kwa utambuzi zaidi.

**MATATIZO YANAYONEKANA MSITU WA BOMBO MASHARIKI 1 NA 2***Peter Juma Ntoglela, Bwana Miti, EUCAMP*

1. Mito ya mara kwa mara.
2. Uvunaji haramu - ukiambatana na ukataji nguzo.
3. Uwindaji wanyama.

**Athari za Matatizo Hayo****Moto**

- a) Uwoto wa asili hutoweka matokeo yake huota miti ambayo haina maana kama Bombo Mashariki 1 na 2 maeneo yaliyoungua yana miti aina ya mishinga.
- b) Unauwa wanyama wadogo wadogo ambao hawana uwezo wa kukimbia.
- c) Kuharibu vyanzo vya maji.
- d) Kuota mimea aina tofauti.
- e) Kuharibu rutuba ardhini.
- f) Kuongezeka kwa panya mashambani.
- g) Kuongezeka kwa wanyama waharibifu mashambani kama nyani, kima, nguruwe sababu yakukosa chakula msituni.
- h) Kuhama kwa viumbe kutoka sehemu moja hadi nyingine.

**Uvunaji Haramu**

- a) Kupotea kwa aina muhimu za miti mfano hapa-mvule.
- b) Kuharibu uoto wa asili na kuuwa mimea iliyojirani na sehemu ulipoangushwa mti.
- c) Kuwepo kwa maeneo ya wazi ndani ya msitu.

**Uwindaji**

- a) Hatari ya moto msituni, wawindaji huwa wanachoma moto na kusababisha wayama kuhamia upande mwingine ili wawapate kwa urahisi - au kuchoma nyama msituni.
- b) Ukataji wa miti aina ya nguzo kufanyia mitego.
- c) Kuuwa wanyama.
- d) Mitego ni hatari kwa watu.

**Tufanye nini ili tuepukane na matatizo haya?**

- Kufanya mikutano ya mara kwa mara na vitongoji vinavyopakana na misitu ya hifadhi.
- Doria za mara kwa mara kushirikiana na wanakamati.
- Kuhamasisha upandaji miti ya matunda, mbao, na kuni - pia kuhamasisha wananchi kulima kilimo cha kuchanganya mazao ya chakula na miti - kilimo mseto au kilimo msitu.

## 7.12: Mgambo Environmental Conservation Workshop Minutes

By Claire Bracebridge, Susannah Hall, Albert Ntemi, Johari Mtango & Amiri Saidi

<b>Date:</b>	18 <sup>th</sup> May 2002
<b>Location:</b>	East Usambara Biodiversity Survey (EUBS) Main camp, Mgambo Catchment Forest Reserve (Bogoro - Bwiti village).
<b>Faciliatators:</b>	Albert Ntemi - EUCAMP Susannah Hall – EUBS Research Co-ordinator
<b>Participants:</b>	EUCAMP Forestry Officers (East Usambara Conservation Area Management Program). EUCAMP Agricultural Extension Officer. EUBS Scientists and Research Assistants. Village <i>mwyenekiti</i> and women from Bwiti Mavovo. Environmental committee members from Bwiti Mavovo and Vuga villages. Villagers of Bwiti Mavovo, Mgambo and Vuga.
<b>Timetable:</b>	
09:00 – 09:15	Opening <i>Gerald Otieno, Forest Officer, EUCAMP</i>
09:15 - 09:20	Welcome to EUBS basecamp <i>Susannah Hall, Research Co-ordinator, EUBS</i>
09:20 - 09:45	Introduction : Eastern Arc & East Usambara forests and importance of reserve areas <i>Albert Ntemi, Biodiversity Officer, EUCAMP</i>
09:45 - 10:45	Current Forest Policy <i>Gerald Otieno</i>
10:45 - 11:00	Break
11:00 - 11:30	Importance of biological research and research methodology of biodiversity surveys <i>Albert Ntemi and Johari Mtango, Agricultural Extension Officer, EUCAMP</i>
11:30 - 12:00	Botanical and zoological specimen viewing <i>Albert Ntemi Susannah Hall and Claire Bracebridge, Assistant Research Co-ordinator, EUBS</i>
12:00 - 12:30	Questions
12:30 - 13:15	Break
13:15 - 14:15	Small group work - conservation issues in Mgambo forest reserve: problem causes, reasons and solutions.
14:15 - 14:45	Group feedback to whole group
14:45 - 15:30	Discussion
15:30 - 15:45	Close <i>Gerald Otieno &amp; Mwenyekiti, Bwiti Mavovo Village</i>

## **1.0 Introduction**

The workshop was opened at 9.30am by Maramba Catchment Forest Officer, Mr Gerald Otieno and the participants were welcomed to the EUBS basecamp by Ms Susannah Hall.

Mr Otieno emphasised to the participants the importance of conserving their environment and the consequences that human daily activities have in influencing environmental destruction.

He stressed that having EUBS main camp located here was a good opportunity to discuss and teach each other, as well as find solutions for environmental problems faced here. He added that co-operation was a vital component in saving our environment.

Mr Otieno thanked the participants for coming to the workshop and invited each to introduce themselves to the workshop, which was carried out before moving on to the introductory speech by Mr Albert Ntemi.

## **2.0 The Eastern Arc**

A map and a short briefing was given to introduce the location and importance of the Eastern Arc mountains. It was explained that the “Eastern Arc” is a chain of mountains that runs from the Taita Hills in Kenya south to the Udzungwa mountains in Iringa, Tanzania. The East Usambaras forests are found in the “Eastern Arc” chain.

Ten million years ago Africa’s forests were a continuous green belt from east to west and north to south. Human activities contributed to the disintegration and fragmentation of these forests. To date agricultural activities are the major cause of forest destruction, creating what are effectively forest “islands”. Daily human activities are still connected to and influence these forest pockets, including the East Usambaras. Therefore, as a group, the importance of the forest and the resulting problems it faced was discussed and the major issues listed for the East Usambaras and particularly locally with respect to Mgambo forest reserve.

### **2.1 The Importance of the East Usambara forests:**

- Employment for timber industries.
- Water catchment areas.
- Shelter for living organisms.
- Weather regulations.
- Medicinal plants.
- Reduction of soil erosion.
- Tourism attractions.
- Source of non timber products.

### **2.2 Problems facing East Usambara Forests:**

Daily human activities which contribute to forest reduction are tree cutting for house building, forest fires and burning, cultivation, timber extraction, grazing and illegal hunting.

### **2.3 Effect of Forest Encroachment:**

- Less trees providing local ecosystem for floral and fauna.
- Reduction of living organisms
- Unreliable rainfall
- Long dry spells.
- Global warming.
- Water pollution.
- Reduction of worship areas.

#### **2.4 Measures taken to save the East Usambara Forests:**

- Introduction of Environmental Conservation to the communities surrounding the forests.
- Conducting forest research and disseminating the findings to the local communities.
- Cooperation between Tanzanian government and NGOs in forest conservation.

### **3.0 Forest Policy**

The forest policy was introduced by the government in 1953 with amendments made in 1963 and 1998 involving all stakeholders. The main reason for involving stakeholders is to increase community participation in forest conservation and sustainable utilisation of natural resources, as they are the main implementors of the forest policy. In order for communities, governmental institutions, international institutions and private organisations to know what to resources to use, they must first know what to conserve.

#### **3.1 Main and Long Term Objectives of the Forest Policy:**

- Strengthen and implement sustainable and equitable use of forest produce for the present and future generations.
- Conserve and monitor forest produce, thereby producing sustainable availability of it.
- Create employment via sustainable forest produce.
- Stabilisation of ecology and forest biodiversity wetlands and soil fertility.
- Increase national monitoring and to develop the national forest sector by involving stakeholders.

#### **3.2 Problems facing the effective implementation of the Forest Policy:**

- Desertation of about 50,000ha per annum.
- Tree harvesting.
- Hunting.
- Animal grazing in the forests.
- Forest encroachment by agricultural activities.
- Stakeholder's rights are not open.
- Poor involvement of stakeholders.
- Poor forest resource monitoring due to inability of government to employ forest technicians.
- Undefined forest borders.

### 3.3 Community Responsibilities:

- To know the forest borders.
- To monitor forest use.
- Provide manpower.

### 3.4 Forest Management

#### Aims:

- The sustainable harvesting of the forest produce.
- To divide the forest into: Government forest
- Local government forest.
- Village forest.
- To conserve biodiversity of the forest.
- To conserve water sources.

#### Strategy:

To make the contracts with the local people and to involve them in the management of the natural resources

### 4.0 Importance of EUBS Biological Research

To look for and identify flora and fauna for the purpose of learning and gaining new knowledge within that topic. To look at cause and effect and provide problem-solving solutions.

Frontier's research is to search for plants and animals such as reptiles, amphibians, rodents and other small animals, and to look at the environment in general within the East Usambaras.

#### 4.1. Objectives:

- To Provide information which will help in planning for the conservation of the forest.
- Training people, including EUCAMP field officers, local villagers and overseas volunteers in field techniques and environmental awareness.
- Provide direction for follow up (i.e. monitoring) research within the forest reserves.

#### 4.2 Advantages:

- To understand the life cycles and ecology of different living organisms in the forest.
- To store information and provide results of the research.
- To publicise the Mgambo forest reserve internationally.
- To provide environmental education to local communities at school and village level.

The East Usambara forests are particularly important because of the living organisms it contains and conserves, especially endemic species, e.g. snakes.

The research helps in understanding rare species obtained in the East Usambaras.

#### 4.3 Methods used for the Research:

- Walking.
- Searching for signs (tracks and dung) of animals.
- Traps.

Before doing anything the forest should be divided into plots of 900 m x 450 m in order to ensure systematic unbiased work, to provide trails to repeatedly use in the forest and to become familiar with the area.

The participants of the environmental workshop were shown some of the equipment used during trapping animals:

Buckets for shrews, snakes, frogs and lizards.

Bat nets for trapping bats.

Sherman traps for rodents e.g. rats, which is baited with coconut and peanut butter.

Butterfly canopy traps, baited with fermented banana.

## **5.0 Problems within Mgambo Forest Reserve: discussion of the environmental workshop:**

Members of the meeting listed problems involved in Mgambo forest reserve:

- Fire.
- Illegal harvesting of forest products.
- Grazing.
- Illegal hunting of animals.
- Lack of widespread environmental education to local communities in general.

### **5.1 Group work:**

The participants divided themselves into three groups for the purpose of discussing the different problems mentioned above and to suggest solutions for them.

### **5.2 Results of discussion groups:**

#### **Group 1**

<b>Problem</b>	<b>Reason/Cause</b>	<b>Solutions</b>
Fire	Hunters Grazers	Restrictions of the illegal hunting activities
Illegal harvesting of forest products	Poor understanding of the meaning of forest reserves	To educate people about the advantage of forest reserves
Grazing	Lack of education	The environmental committees will educate the hunters
Lack of education in understanding the forest	Insufficient training	To get education from the environmental committees

**Group 2**

<b>Problem</b>	<b>Source/ Causes</b>	<b>Solutions</b>	<b>Persons responsible to implement solutions</b>	<b>Tools/ Equipment needed</b>
Fire	Hunters Honey Hunters	Fire breaks Road construction Mass education on effects of fire	Villagers	Tools to construct a road and dig fire breaks.
Illegal Harvesting of Forest Products	The desire to acquire money	Take them to the village office	Chair person	Small laws and law enforcement
Grazing	Lack of grazing areas outside of the reserves	Village government to allocate areas	Village to government	Environmental committees
Hunting	Desire / need for meat / food	Take them to the village office	Villagers	Patrols
Lack of Education in the understanding of the forest reserve.	Poor participation of local people	To involve the stakeholders	Villagers and the village government	Education

**Group 3**

<b>Problem</b>	<b>Reason / Cause</b>	<b>Solution</b>
Fire	Shamba Grazing Hunting Unkept borders Honey Charcoal	Good shamba preparation will help to control fires. Zero grazing or provide alternatives, such as herd reduction, planting grass or improved land use in the village. Clear borders Introduce bee keeping in shambas Use kerosene and other fuel alternative to charcoal. General law enforcement.
Tree Harvesting and Forest Produce	Poverty No trees suitable outside of the forest. Population increase Development – housing, etc.	Income generating activities (government) – group action / interest. Plant trees in the shambas. Population control – condoms. Buy timber. Law enforcement.
Grazing	No area set aside for	Improved land use in village (Muheza) –

	grazing.	collective action. Grow grass. Reduce livestock. Have chickens / duck not cows or goats. Law enforcement.
Hunting	Lack of meat / poverty	Keep chickens / ducks to reduce the dependence on forest meat.
Lack of Education about the Forest	Lack of money – government. Lack of personnel – government.	Government search for external funding and/ or utilise NGOs. Collective action i.e. from villagers to local and district levels of government, as well as more centralised action.

## 6.0 Discussion

One of the villagers tried to explain the past procedures used, such as different pasture areas and different areas for watering the animals. There are areas reserved as pasture but the problem is the way / access to the area. Some of these areas are no longer accessible due to shambas.

Environmental protection is important for the local people surrounding the Mgambo forest. The villagers felt strongly about the need to conserve their natural resources in the forest.

### 6.1. Suggestions for future positive action / aims:

- They want to prohibit the grazing of animals in the reserve and drinking from the streams in the forest.
- Any illegal activities should be reported to the leaders. Such reports should not be hidden.
- Mass education to people is required in order to feel that the forest belongs to them and that it is their responsibility to ensure no destruction occurs. If it does, it is up to them to solve the problems and produce a positive outcome.
- The laws governing the forest are important to be used as required and enforced by all leaders.
- There is poor performance for those environmental committees to date. It would be better if the committees have more power over daily activities.

All participants of the workshop were finally informed that on 8<sup>th</sup> June 2002 there would be a World Environmental Day event. Frontier will participate in this in Bwiti village. Members of this workshop are requested to advertise this to the villagers to encourage participation in this day at Bwiti Primary school.

Any villagers with any ideas or opinions for environmental conservation are welcome to the office with an opportunity to discuss their ideas and contribute to the day.

### **7.0. Closing Speech**

Bwiti *mwenyekiti* closed the workshop at 4.12 pm by thanking the participants and Frontier staff for their good contribution to the days discussions. Moreover he emphasised the worth of researchers exchanging their ideas with locals for environmental conservation issues.

### 7.13 Warsha ya uhifadhi wa mazingira msitu wa hifadhi Mgambo Usambara Mashariki

*Na Claire Bracebridge, Susannah Hall, Albert Ntemi,, Johari Mtango & Amiri Saidi*

<b>Tarehe:</b>	18 Mei 2002
<b>Mahali:</b>	Kambi Kuu ya EUBS – Msitu wa Hifadhi Mgambo (Bogoro – Kijiji cha Bwiti)
<b>Wawezeshaji:</b>	<i>Albert Ntemi - EUCAMP</i> <i>Susannah Hall – Frontier-Tanzania</i>
<b>Washiriki:</b>	Ofisi ya hifadhi misitu – Mabwanamiti , Bwanakilimo Wataalamu kutoka EUBS Wenyeviti wa vijiji – Bwiti Mavovo Wajumbe wa kamati za Mazingira – Bwiti Mavovo Wanavijiji toka Bwiti Mavovo na Vuga
<b>Ratiba:</b>	
3:00 – 3:15	Kufungua Washa – Mkuu wa Kituo cha Misitu Maramba- <i>Gerald. Otieno</i>
3:15 – 3:20	Makaribisho <i>Susannah Hall</i>
3:20 – 3:45	Utangulizi:- Milima ya Ukanda wa Mashariki na Misitu ya Usambara Mashariki <i>Albert Ntemi.</i>
3:45 – 4:15	Sera mpya ya misitu <i>Gerald Otieno</i>
4:15 – 5:00	Chai
5:00 – 5:30	Umuhimu wa Utafiti wa Viumbe Adimu na Mbinu zitumikazo katika utafiti <i>Albert Ntemi na Johari Mtango</i>
5:30 – 6:00	Kuona sampuli za wanyama na mimea <i>Albert Ntemi, Susannah Hall na Claire Bracebridge</i>
6:00 – 6:30	Maswali
6:30 – 7:15	Chakula
7:15 – 8:15	Kazi za Vikundi – Masuala ya Uhifadhi katika Msitu wa Hifadhi Mgambo – Chanzo cha matatizo, sababu, na hatua za kuchukua.
8:15 – 8:45	Matokeo kutoka kila kikundi
8:45 – 9:30	Majadiliano – Wote
9:30 – 9:45	Kufunga <i>Gerald Otieno &amp; Mwenyekiti wa Kijiji, Bwiti</i>

### **1.0 Utangulizi, Makaribisho:**

Kikao kilifunguliwa na Afisa Misitu wa Maramba, Bwana Otieno, saa 3:20 Asubuhi. Alianza kwa kuwataarifu wajumbe namna ya uhifadhi misitu. Mazingira na Shughuli za binadamu zimesababisha kuharibu mazingira kwa kiasi kikubwa.

‘Leo tumefika katika Kambi ya Utafiti hivyo ni wakati mzuri wa kukutana na kujadiliana mambo mengi. Tushirikiane katika kufundisha.’ Alimaliza kwa kuwashukuru wajumbe kwa kufika.

Bwana Mtango aliwataka washiriki wajitambulishe, jambo lililofanyika kabla ya ndugu Albert Ntemi kutoa hotuba ya utangulizi.

### **2.0 Milima ya Ukanda wa Mashariki:**

Alianza kwa kuonyesha wanawarsha ramani ya Milima ya Safu ya Mashariki, kuanzia milima ya Taita-Kenya, hadi milima ya Udzungwa-Iringa, Tanzania. Ndani ya ukanda huo wa safu ya Milima ya Ukanda wa Mashariki ndimo ilimo milima ya Usambara Mashariki.

Miaka milioni kumi iliyopita misitu ya Afrika ilikuwa imeungana. Shughuli za kila siku za binadamuzimechangia sana kuitenganisha misitu hii, na kuifanya iwe inaonekana kama visiwa. Misitu ya Usambara Mashariki ni misitu ambayo inahusishwa na Shughuli za kila siku za binadamu.

#### **2.1 Umuhimu wa Misitu Hii:**

- Ajira katika viwanda vya mbao
- Kuhifadhi vyanzo vya maji
- Makazi ya viumbe hai
- Kurekebisha hali ya hewa
- Dawa za Asili
- Kupunguza mmomonyoko wa udongo
- Kivutio kwa watalii
- Chanzo cha bidhaa zitokanazo na mbao

#### **2.2 Matatizo yanayoikabili Misitu ya Usambara Mashariki:**

Shughuli za kila siku za binadamu zimechangia kuhatarisha kutoweka kwa misitu hii. Mf. Ukataji kuni, uchomaji moto, n.k.

#### **2.3 Athari Zake:**

- Miti michache yenye kutupatia ikolojia kwa mimea na wanyama
- Kupungua kwa viumbe hai
- Mvua isiyotegemewa
- Ukame wa mara kwa mara
- Ongezeko la joto duniani
- Uchafuzi wa maji
- Kupungua kwa maeneo ya kuabudia

#### **2.4 Nini Kifanyike Kuokoa Misitu ya Usambara Mashariki:**

- Elimu ya Mazingira kwa umma.
- Utafiti na kutoa ushauri kwa umma.

- Serikali pamoja na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kushirikiana katika utunzaji wa misitu.

### **3.0 Sera Mpya ya Misitu:**

Sera ya Misitu ilianzisha na serikali 1953 na kurekebishwa 1963 na 1998 kwa kuwahusisha washikadau. Sababu kubwa ya kuwahusisha washikadau ni kuongeza ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi wa misitu kwa matumizi endelevu ya maliasili, kwani wao ndio watekelezaji wakubwa wa sera hii. Ili jamii, taasisi za serikali, taasisi za kimataifa, na mashirika binafsi kujua ni raslimali kiasi gani kutumia, lazima yajue ni kiasi gani kuhifadhi.

### **3.1 Malengo Makuu na ya Muda Mrefu ya Sera ya Misitu:**

- Kuimarisha na kutekeleza matumizi endelevu na linganifu ya mazao ya msitu kwa kizazi cha sasa na vijavyo.
- Kutunza na kulinda mazao ya msitu, ili kuhakikisha uwepo wake.
- Kupanua ajira kwa kuendeleza uwepo wa mazao ya msitu
- Kuimarisha mfumo wa ikolojia, biyoanuwai ya misitu na vilindimaji, na rutuba ya udongo.
- Kukuza uwezo wa taifa katika usimamiaji na kuendeleza sekta ya misitu ya taifa kwakushirikiana na washikadau.

### **3.2 Matatizo ya Utekelezaji wa Sera ya Misitu:**

- Ukuaji wa jangwa kwa kasi ya hekta 50,000 kwa mwaka
- Uvunaji wa miti
- Uwindaji
- Ulishaji mifungo misituni
- Uvamizi wa misitu ufanywao na wakulima
- Haki za washikadau haziko wazi
- Ushirikishwaji mdogo wa washikadau
- Udhhibiti duni wa raslimali za misitu utokanao na serikali kukosa uwezo wa kuajiri wataalamu wa misitu.
- Mipaka ya misitu haijabainishwa vizuri.

### **3.3 Majukumu ya Jamii:**

- Kujua mipaka ya msitu
- Kusimamia matumizi ya msitu
- Kutoa nguvukazi

### **3.4 Usimamizi wa Misitu, Madhumuni:**

- Upatikanaji na uvunaji endelevu wa mazao ya msitu.
- Kugawa misitu katika: Misitu ya Serikali Kuu  
Misitu ya serikali za mitaa  
Misitu ya vijiji
- Kuhifadhi bayoanuwai ya msitu.
- Kuhifadhi vyanzo vya maji

### **Mikakati:**

Kuweka makubaliano na wenyeji na kuwahusisha katika udhibiti wa maliasili.

#### 4.0 Umuhimu wa Utafiti wa Kibayolojia wa Frontier Tanzania

Maana ya Utafiti: Ni kuchunguza, kufuatilia ili kujua mambo Fulani (mf. Matatizo, sababu, matokeo, n.k.) na kutoa ushauri wa kuondoa matatizo hayo.

Utafiti wa kikundi cha Frontier kwenye misitu ya Usambara zaidi ni utafiti wa mimea na viumbe, mf. Wadudu, wanyama, ngege, mimea, hali ya mazingira, n.k.

#### 4.1 Malengo:

- Kutoa taarifa zitakazosaidia kuendeleza kupanga mipango ya uhifadhi bora wa misitu
- Kutoa mafunzo kwa wataalamu mbalimbali wa misitu, wananchi, n.k.
- Kutoa mwelekeo wa ufuatiliaji wa shughuli za misitu

#### 4.2 Faida:

- Kufahamu aina ya viumbe hai vilivyomo ndani ya maeneo ya misitu.
- Kuweka kumbukumbu za matokeo.
- Kutangaza msitu wa Mgambo katika ngazi ya kimataifa.
- Kutoa elimu katika ngazi ya shule na vijiji.

Umuhimu wa misitu ya Usambara Mashariki ni kwa jinsi misitu hii inavyoweza kuhifadhi viumbe wa pekee ambao hawapatikani mahali pengine duniani, mf. Nyoka, vinyonga, n.k. Utafiti huu umetuwezesha kufahamu viumbe adimu vilivyomo Usambara Mashariki.

#### 4.3 Mbinu Zinazotumika katika Utafiti:

- Kutembea
- Kutafuta ishara (nyayo na vinyesi) vya wanyama
- Mitego

Kabla ya kufanya chochote msitu hugawanywa katika vieneo vya m 900 x m 450 ili kuhakikisha kazi inafanyika kwa utaratibu na bila upendeleo, na pia kuweka njia za kutumia mara kwa mara msituni kuujuu vizuri msitu.

Washiriki wa warsha walionyeshwa baadhi ya vitu vitumikavyo katika kutega wanyama:

- nazi na karanga kwa ajili ya panya
- ndizi kwa ajili ya vipepeo
- ndoo – kupata panya, nyoka, chura, mijusi, n.k.
- Neti - kupata popo

#### 5.0 Matatizo ndani ya Msitu wa Hifadhi Mgambo:

Washiriki walitaja matatizo yaliyomo Msitu wa Hifadhi Mgambo.

- Moto
- Uvunaji haramu wa mazao ya msitu
- Ulishaji mifugo
- Uwindaji haramu
- Ukosefu wa elimu pana ya mazingira kwa jamii enyeji kwa ujumla.

### 5.1 Kazi za Vikundi:

Washiriki walijigawa wenyewe katika makundi matatu kwa nia ya kujadili matatizo mbalimbali yaliyotajwa hapo juu na kutoa ushauri wa nini kifanyike kupata suluhisho.

### 5.2 Matokeo ya Majadiliano:

#### Kikundi 1

Tatizo	Sababu	Suluhisho
Moto	Wawindaji Wachungaji	Wasiwinda eneo la hifadhi
Uvunaji haramu wa mazao ya msitu	Kutoelewa maana ya kuhifadhi misitu	Kuwaelimisha wananchi juu ya faida ya kuhifadhi misitu
Ulishaji mifugo	Ukosefu wa elimu	Ni kuwadhibiti wenye mifugo kwani tunawafahamu
Uwindaji	Ukosefu wa elimu	Kamati ya mazingira itachukua jukumu la kuwaelimisha wawindaji
Ukosefu wa elimu katika kuelewa misitu	Kukosa mafunzo wataalamu	Kuelimishwa na kamati ya mazingira

#### Kikundi 2

Tatizo	Chanzo/ Sababu	Kutatua Tatizo	Mhusika	Nyenzo inayohitajika
<b>Moto</b>	Wawindaji Walina asali	Kulima barabara. Kuelimisha watu kuhusu adhali za moto	Mwanakijiji Mwenyewe	Kulima njia
Uvunaji wa mazao ya msitu ovyo	Tamaa ya pesa	Apelekwe kwenye ofisi ya kijiji	Mhusika wa kijiji ambaye ni mwenyekiti	Sheria ndogo
Kuchunga Mifugo	Kukosa maeneo	Kijiji kiwapatie maeneo	Serikali ya kijiji	Kamati ya mazingira ya kijiji
Uwindaji	Uchu wa nyama	Apelekwe ofisini	Mwananchi	Doria
Ukosefu wa elimu ya Ufahamu kuhusu Msitu wa Hifadhi	Kutoshirikishwa	Wadau na wataalamu washirikiane	Mwananchi na serikali ya kijiji	Elimu

**Kikundi 3**

<b>Tatizo</b>	<b>Sababu</b>	<b>Suluhisho</b>
Moto	Shamba –mkaa Ulishaji mifugo Uwindaji -kulina asali Mipaka isiyotuzwa	Uandaaji mzuri wa mashamba utasaidia kuzuia mioto. Ufugaji wa ndani au upunguzaji mifugo, upandaji majani au kuboresha matumizi ya ardhi kijijini. Kusafisha mipaka Kuanzisha ufugaji wa nyuki mashambani Kutumia mafuta ya taa au nishati nyingine mbadala Kutilia mkazo sheria kwa ujumla
Uvunaji miti na mazao ya msitu	Umasikini Hakuna miti ifaayo nje ya msitu Ongezeko la watu Maendeleo-ujenzi, n.k.	Shughuli za kuongeza kipato (serikali) Kupanda miti mashambani Kudhibiti ongezeko la watu—kondomu Kununua mbao Kutilia mkazo sheria
Kuchunga Mifugo	Hakuna maeneo yaliyotengwa kwa malisho	Kuboresha matumizi ya ardhi vijijini (Muheza) – juhudi za pamoja. Kuotesha majani Kupunguza mifugo Kufuga kuku/bata badala ya ng'ombe au mbuzi Kutilia mkazo sheria
Uwindaji	Uhaba wa nyama/ umasikini	Kufuga kuku/bata kupunguza utegemezi wa nyama ya porini.
Ukosefu wa mwamko juu ya misitu	Ukosefu wa fedha (serikali) Ukosefu wa wataalamu (serikali)	Serikali itafute fedha nje na/au iimarisha NGOs. Juhudi za pamoja k.v. kutoka kwa wanakijiji kwenda serikali ya mtaa na wilaya.

**6.0 Majadiliano:**

Mwanawarsha mmoja alijaribu kuelezea utaratibu uliokuwepo zamani. Maeneo ya kuchungia mifugo yalitengwa, maeneo ya kunyweshea mifugo na hata njia maalum za kupitishia mifugo zilikuwapo. Hivyo ni vyema viongozi pamoja na wananchi wakae pamoja ili kurudisha utaratibu uliokuwepo zamani.

Vilevile wajumbe walieleza kwamba maeneo ya kulishia mifugo yapo na yametengwa tangu siku nyingi. Tatizo ni njia ya kupitisha mifugo. Elimu ya mazingira ni muhimu kwa wanajamii wanaozunguka Msitu wa Mgambo. Wajumbe waliombwa kuwa na uchungu na msitu wao. Washirikiane na serikali za vijiji pamoja na wataalamu wa misitu waliopo.

**6.1 Mapendekezo kwa mafanikio ya baadae:**

- Wanahitaji kuzuia uchungaji mifugo ndani ya eneo la hifadhi na kunywesha mifugo kwenye vijito msituni.
- Shughuli haramu yoyote iripotiwe kwa viongozi. Taarifa hizo zisifichwe.

- Elimu kwa jamii inahitajika ili kuifanya ijihisi msitu ni wake na inawajibu wa kuhakikisha hauharibiwi. Ukiharibiwa basi ni jukumu lao kuurudisha katika hali yake ya kawaida.
- Sheria zinazohusu misitu ni muhimu kutumika na kutiliwa msisitizo na viongozi wote.
- Kunautendaji kazi duni wa kamati za mazingira kwa sasa. Ingekuwa vizuri kama kamati zingekuwa na mamlaka zaidi katika Shughuli za kila siku.

Washiriki wote wa warsha hii mwishoni walijulishwa kuwa tarehe 8 juni 2002 kutakuwa ni Siku ya Mazingira Duniani. Frontier itashiriki katika tukio hili katika kijiji cha Bwiti. Wajumbe wa warsha hii wanatakiwa kulitangaza tukio hili kwa wanavijiji kuwahamasisha washiriki siku hiyo hapo Shule ya Msingi Bwiti.

Kila mwanakijiji mwenye mawazo au maoni juu ya uhifadhi wa mazingira anakaribishwa ofisini kwa nafasi ya kuyajadili mawazo yake na kuchangia katika siku hiyo.

### **7.0 Kufunga:**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Bwiti alifunga warsha saa 10.12 jioni kwa kuwashukuru washiriki na wafanyakazi wa Frontier kwa michango yao mizuri katika majadiliano. Zaidi ya hapo alisisitiza umuhimu wa watafiti kubadilishana mawazo na wenyeji katika masuala ya uhifadhi wa mazingira.

### **7.14: Maramba Secondary School, Visit to Mgambo Forest Reserve Frontier Basecamp, 4<sup>th</sup> May 2002**

- 8.30 a.m. Welcome to camp.  
Group shown round tents, eating area, science banda etc.
- 9 a.m. Forest Reserve/Conservation Talk:  
-Importance of East Usambaras within Eastern Arc/world  
-Concept/reasons for Nature and Forest Reserves/Buffer Zones  
-Threats to the forests and conservation issues
- 10.30a.m. - 11 a.m. Tea break**
- 11 a.m. - 12.30p.m. Frontier/Biodiversity Talk/Activities  
-Discuss plant/animal diversity within the East Usambaras  
-Introduce some sampling techniques and specimens  
-Walk through Riverine Forest looking for monkeys/frogs/birds, discussing issues, plants etc. as go. Walk to 'set-up' of trapsite to demonstrate capture techniques (take binoculars for students).
- 12.30p.m. - 1.30 p.m. Lunch**
- 1.30 p.m. - 2.15p.m. 'Environment Day' Plans  
-Discuss concept of World Environment Week and proposed Environment Day (Bwiti, 8<sup>th</sup> June). Ideas for Maramba School's involvement (posters, poems, plays, songs). Theme for the Day is to be 'how each individual can make a positive difference to the environment'. Write suggested topics/issues on white board.
- 2.15p.m. - 2.30p.m. Photos, 'Thank yous' etc.
- 2.30 p.m. Close

**7.15: Ratiba ya siku ya Mazingira Bwiti****8<sup>th</sup> June, 2002**

Muda	Shughuli	Mhusika
8.00	Ufunguzi wa Siku ya Mazingira na kutambulisha wengi	Mwenyekiti wa kijiji Bwiti
8.15	Nyimbo, ngonjera na mashairi kutoka shule ya msingi Bwiti (ngoma)	Shule ya msingi Bwiti
9.00	Kwaya na shairi kutoka shule ya sekondari Maramba	Shule ya sekondari Maramba
10.00	Hotuba ya mgenirasmu Zawaidi kwa mshindi wa michoro ya mabango	Katibu tarafu Katibu tarafu
10.30	Mchezo wa kirafiki (Frontier na Bwiti)	
11.45	Kufunga Siku ya Mazingira	Katibu tarafu